TOLEO NO.61

# Khilafah

(SHAWWAL 1446 HIJIRIA —APRILI 2025 MILADIA) ( Bei  Tsh 2,000/= - Ksh 100/=)

NDIO SULUHISHO













Yaliyomo :


- Maradhi Ya Saratani katika Ubepari  uk....2
- Ramadhani imeisha majukumu bado uk...3
- Malipo ya deni lililopita muda uk…………4
- Ukoloni  wa sarafu ya Dolari uk…………...7
- Watuhumiwa wa ugaidi waachiwe  uk…...8
- Uislamu na ‘Hatimiliki’ uk……... 5
- Ukoloni  wa sarafu ya Dolari uk...7



Karibuni Wizara ya Afya Zanzibar wakati ikiwa na mazungumzo na taasisi ya Wakala wa Kimataifa wa Nguvu za Atomu IAEA kupitia mwakilishi wake Profesa Peter Knoll na Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania TAEC ilitoa tamko kuwa katika kukabiliana na changamoto za maradhi ya saratani Wizara hiyo kwa kushirikiana na taasisi hizo inakusudia kuanzisha Hospitali ya maradhi ya saratani Zanzibar kwa lengo la kukabiliana na maradhi hayo.

Saratani ni katika majanga makubwa yanayoikabili Zanzibar bali yanayoikabili Tanzania kwa ujumla. Kwa mujibu wa taasisi ya Mpango wa Rais wa Zanzibar wa Kukabiliana na Saratani (Zanzibar Presidential Cancer Initiatives) inakadiriwa kuwa kila mwaka. Kuna zaidi ya watu 400 wanaopata Saratani Zanzibar na watu 83 hufariki dunia kwa mwaka.

https://www.facebook.com/permalink.php/?stry_fbid=1050390913760246&id=100063680411201

Aidha, kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Masuala ya saratani Zanzibar Dr. Msafiri Marijani inakadiriwa kiasi cha watu 1000 kutoka visiwani Zanzibar hupokelewa kila mwaka katika hospitali ya ya saratani ya Ocean road kwa ajili ya matibabu.

Na kwa nchi nzima, hugundulíwa wagonjwa wapya wa saratani takriban 40,000 kila mwaka

na karibu watu 27,000 hufariki dunia. https://www.moh.go.tz/news-single/wagonjwa-wapya-wa-saratani-40-elfu-hugundulika-kila-mwaka-vifo-27-elfu

Saratani maarufu zaidi znazoathiri afya na zinazoongoza kuathiri wengi ni pamoja na saratani ya matiti, saratani ya mlango wa kizazi, tezi dume nk.

Kuna hatua kadhaa kitaifa zinazochukuliwa katika kukabiliana na janga la saratani ikiwemo kuasisiwa taasisi mbali mbali, kuongezwa vituo vya uchunguzi, vituo kuwezeshwa kifedha kama alivyotangaza raisi mwishoni mwaka jana mpango wa serikali kutoa kiasi cha Sh169 bilioni ili kuviimarisha vituo vilivyopo na kuongeza vituo vipya vya saratani kwa teknolojia ya nyuklia nk.

Pamoja na changamoto mbali mbali katika kukabiliana na janga la maradhi ya saratani kama ukosefu wa wataalamu,wa kutosha katika vituo vya afya, ukosefu wa vifaa tiba, dawa za tiba na uelewa mdogo wa jamii

**Inaendelea uk. 4**

# RAMADHANI IMEISHA—MAJUKUMU YANAENDELEA

Alhamdullilah, tumemaliza mwezi mtukufu wa Ramadhani uliojaa kheri nyingi mno, na leo tupo katika Sikukuu ya Eid ul-Fitri yenye baraka.

Jarida la Khilafah linatoa hongera na salamu za dhati kwa Umma mzima wa Kiislamu ulimwenguni kote kwa kuingia katika siku hii tukufu. Allah SWT Atulipe malipo adhimu kwa Swaumu zetu na Ajaalie Eid yetu iwe iliyosheheni faraja na furaha. Amiin.

Wakati baadhi yetu tukiwa katika furaha ya Eid, sehemu ya Umma wetu katika Gaza uko mbali na hali hiyo kutokana na dhulma, mateso, mauaji ya halaiki na idhilali kutoka kwa mayahudi kwa msaada na baraka za Marekani.

Hawajasita wala hawatosita makafiri licha ya kuwa wameshatenda mauaji ya kikatili ya halaiki ya zaidi ya watu 50,000 na kujeruhi wengi katika wanawake, watoto na wazee.

Yanatendeka mauaji na dhulma hizo mbele ya macho ya watawala vibaraka wa nchi za Waislamu kama Misri, Jordan,

Uturuki, Saudia, Iran nk. Kama kawaida yao wakitoa macho tu au kutoa kauli tupu bila ya vitendo..

Aidha, Umma wetu katika maeneo mengine kama Sudan, Kashmiri, Turkistan ya Mashariki, Burma, maeneo yetu Afrika ya Mashariki nk. wengine wamo katika vita, wanakabiliwa na mateso, kuzuiliwa kufunga, kuwekwa vizuizini kwa kisingizio cha ugaidi nk.

Bila ya kusahau pia kwamba wakati tukiingia katika Eid sehemu ya Umma wetu pia inasibiwa na njaa, unyonge na umasikini licha ya rasilmali nyingi katika ulimwengu wa Kiislamu ambazo hazinufaishi Umma ipasavyo, zaidi ya kuporwa na madola ya kibepari.

Pamoja na ugumu wote na hali ya jamii kuzingirwa na maovu na, ibada ya Swaumu kufanyiwa kampeni ya kukebehiwa kwa kufanywa kuwa jukwaa la kutangaza 'dini mseto' na kupigia debe wasanii wanaobeba ajenda za uharibifu katika jamii, bado Waislamu wamefunga kwa mapenzi, ucha Mungu,subra na yakini, na wengi kukemea kutumika vibaya ibada hii kwa malengo ya ukafiri. Alhamdullilah, hii ni dalili njema kwa Umma wetu.

Tunachukua fursa hii kuwakumbusha Waislamu kwamba ibada haikumalizika kwa kumalizika Ramadhani, kwa kuwa kila tendo ni ibada na ndio lengo la uwepo wetu hapa duniani.

Aidha, tunawakumbusha Waislamu kama tulivyobeba faradhi ya Ramadhani ambayo inakuja mara moja kwa mwaka, ndivyo vivyo hivyo tunavyopaswa kuzibeba faradhi nyengine zote na muda wote.

Na taji la faradhi zote ni kurejesha tena maisha ya Kiislamu kwa kupitia kurudisha tena dola ya Kiislamu ya Khilafah inayopaswa kuanzia katika ulimwengu wa Kiislamu na kuenea kila mahala. Dola hiyo ndio tiba ya kukabiliana na kuondoa mashaka yote yanayousibu Umma wetu, iwe Gaza, Sudan, Yemen au penginepo.

Basi kumalizika kwa Ramadhani kuwe mwanzo mpya wa kuamsha ari, hima na ghera ya kweli ya kulibeba jukumu hilo adhimu la kufa na kupona

**Mhariri**

**01 Shawwal 1446 Hijria**

**30 Aprili 2025 M**

***jukwalakhilafah@gmail.com***

USIKOSE KUSOMA JARIDA LAKO LA KHILAFAH KILA MWEZI

## Malipo ya Deni lililopita Muda

**Swali:**

Ni nani anaebeba mzigo wa tofauti thamani ya sarafu ikiwa mkopaji amechelewa kulipa deni kwa mkopeshaji bila sababu, kwa mfano, miaka kumi, ima deni liwe ni mshahara au mkopo.

**Jibu:**

Mshahara unaofaa kulipwa (ambao umecheleshwa) ni kama deni. Yeyote anayedaiwa na mtu mwengine ni lazima kutimiza kulipa kwa mujibu wa makubaliano kati yao. Lau mkopaji/ mdaiwa atachelewa katika kulipa deni, huzingatiwa: ikiwa amekabiliwa na uzito, basi anayedai lazima ampe muda mpaka ajimudu hali yake ya kifedha na aweze kulipa deni kama alivyosema Mwenyezi Mungu (swt):

وَإِن كَانَ ذُو عُسْرَةٍ فَنَظِرَةٌ إِلَىٰ مَيْسَرَةٍ

***"Na akiwa mdaiwa ana shida, basi (mdai) angoje mpaka afarijike.*** **[Al-Baqara: 280]**

Ikiwa mdaiwa ana uwezo wa kulipa lakini asilipe deni lake analazimishwa kulilipa na akikataa ataadhibiwa kwa mujibu wa alivyosimulia Abu Dawud na Ibn Majah kutoka kwa 'Amr bin Sharid kutoka kwa babake kwamba Mtume (saw) alisema:

لَيُّ الْوَاجِدِ يُحِلُّ عِرْضَهُ وَعُقُوبَتَهُ

***"Yeyote ambaye ana uwezo wa kulipa deni lakini akachelewa kulipa, heshima na adhabu yake imeruhusiwa."***

Maana ya "Lai Alwajd" katika Hadith ni kuchelewa kwa tajiri, maana ya heshima yake imeruhusiwa ni kumlalamikia na kumkemea kwa maneno, na maana ya adhabu yake ni kufungwa na kuwekwa kizuizini.

Amma kuhusu tofauti katika sarafu yaani thamani yake kupungua au kuzidi ikilinganishwa na dhahabu au fedha katika bei ya soko, na anayebeba mzigo wa tofauti ya thamani. Kwa mujibu wa rai yenye nguvu kwa mtazamo wangu ni kuwa ulipaji wa deni uwe kwa sarafu ile ile (waliyokopeshana) na kiwango kiwe kile kile ambacho kimethibitishwa katika deni ili kuepuka riba endapo utachukua kiwango cha zaidi. Hii ni ikiwa sarafu ipo katika mzunguko na inatambulika rasmi na taasisi iliyoiidhinisha.

Na ikiwa mkopeshaji anataka kuhifadhi pesa zake kutokana na kupungua thamani, basi (tangu awali) alipaswa akopeshe kwa dhahabu au sarafu yenye nguvu iliyo na uwezo wa kubakisha thamani yake.

**Mwenyezi Mungu ni Mjuzi, Mwenye Hekima.**

**Majibu ya maswala haya hujibiwa na Amiri wa Hizb ut Tahrir ( Allah Amhifadhi) na hupatikana katakana katika**

**TUNAWATAKIA WAISLAMU KILA LA KHERI KWA KUINGIA SIKU ADHIMU YA EID EL -FITR**

*Saratani –kutoka uk..2*

juu ya kujikinga na saratani, bado tatizo kubwa la msingi ni la kisera nzima katika sekta ya afya. Iwe katika kukabiliana na saratani au maradhi mengineyo.

Sera ya afya ambayo nchi zetu iwe Zanzibar na nchi zote changa kwa jumla zinatokana na kuigiza mfumo wa kibepari, ambapo zimezigeuza huduma za kijamii ikiwemo afya kuwa ni huduma ya kibiashara. Hii ni kutokana na maumbile ya mfumo wa kibepari kukiangalia kila kitu katika mtazamo wa kimaslahi. Aidha, kazi ya serikali katika ubepari husukumwa na msukumo huo wa kimaslahi, iwe kwa wanasiasa au sera za serikali, japo wanasiasa wa kibepari hudai kwamba wapo kuwatumikia raia, lakini uhalisia wapo kuchunga maslahi yao na sio kingine.

Kwa hivyo, chini ya sera za kibepari uwepo wa vituo vingi vya kutibu saratani, kuviwezesha kifedha, kuanzisha miradi mingi mikubwa kwa ajili ya maradhi hayo kamwe hakutotatua tatizo katika msingi wake, na wanyonge na wananchi wa kawaida hawatopata takhfifu wataendelea kukosa huduma hizo na kuumia kutokana na hali zao za kipato kidogo.

*Inaendelea uk.6*

## UFAHAMU WA KIISLAMU JUU 'HATIMILIKI'

Kila tarehe 26 Aprili ya kila mwaka ni siku ya kimataifa ya Milki za Kifikra (World Intellectual Property Day).

Maana ya milki za kifikra ni kama ubunifu, uvumbuzi, wazo, fikra, maarifa anayoyatoa mtu binafsi, kikundi au taasisi.

Miongoni mwa dhana inayotumika kuhifadhi milki za kifikra ni dhana ya "hati miliki"

Hii ni dhana inayokusudiwa kuhifadhi umiliki wa fikra, wazo au uvumbuzi wa kimaandishi wa mtu kwa kumzuiya mtu mwingine asiyekuwa mtoa wazo hilo kuiga, kutawanya au kutumia wazo hilo bila ya idhini ya mzaa wazo hilo au mbunifu wa fikra hiyo wa asili.

Hatimiliki wameweka wamagharibi katika kuendeleza ukoloni, uchoyo, ukiritimba na roho mbaya katika kuenea maendeleo duniani kwa usahali na kwa haraka.

Lau kama si dhana hii katili ya hatimiliki huenda dunia ingekuwa katika hali ya ajabu ya sayansi na teknolojia.

Kabla ya kufafanua mtazamo wa Kiislamu juu ya hatimiliki ni muhimu kufahamu namna mtazamo wa kibepari unavyolifafanua na unavyoonesha sura ya jambo hili :

a. Hati miliki ya mtu ni milki yake kama milki nyingine za mwanadamu kama vitu vya kushikika kama nyumba, gari, nk.

b. Hatimiliki ni miongoni mwa mambo yanayosimamiwa kimataifa chini ya shirika maalumu la Umoja wa Mataifa linalojihusisha na uhifadhi wa milki za kifikra linaloitwa World Interlectual Property Organization (WIPO) lililoundwa mwaka 1967, lenye wanachama 193 ikiwemo Tanzania. Lengo la shirika hilo ni kuhamasisha ulinzi wa milki za kifikra duniani ikiwemo suala la hati miliki.

c. Haki miliki ya mtu inalindwa kisheria ulimwenguni kote, na kuna sheria nyingi zimetungwa kuhifadhi milki hiyo. Kwa mfano, Tanzania ina sheria maalumu inayoitwa Copyright and Neighbouring Rights Act.5. Na taasisi inayoitwaThe Copyright Society of Tanzania (COSOTA) ndio taasisi yenye dhamana ya usimamizi wa masuala ya hati miliki.

D.Haruhusiwi mtu mwengine ktumia au kunufaika na milki hiyo ya kifikra, kielimu au kiubunifu bila ya idhini ya mmiliki asili.

**Uislamu na Hatimiliki**

Uislamu haukubali wala hautambui dhana ya hatimiliki kwa sababu zifuatazo:

1. Inadumaza akili za watu na ni kipingamizi cha ubunifu au kuzidisha ubora juu ya kitu kilichobuniwa na mwingine.

2. Dhana hii inapingana na uhalisia wa maisha ya wanadamu. Kwa sababu wanadamu katika dunia wamekuwa wakitegemeana katika ubunifu na uvumbuzi. Kinachodhihirika ni kuwa wakati wote wanadamu hufanya ubunifu na uvumbuzi, na wanadamu wengine huja kuzidisha au kuboresha elimu au ubunifu wa waliomtangulia tokea zama za binadamu wa mwanzo. Mfano hai, nchi za magharibi waliiba vitabu vingi vya wabunifu na wavumbuzi wa Kiislamu ambavyo vimewaongoza katika ubunifu wa mambo mbali mbali. Kwanini wavumbuzi wapya nao wasilipe kwa wavumbuzi na wabunifu waliotangulia ?

3. Dhana hii ina dhulma, kwa sababu inampokonya umiliki wa dhati kwa mtu. Mathalan, vipi mtu aliyenunua kitabu, lakini kwa mujibu wa fikra ya hatimiliki hana haki ya kukichapisha nakala zaidi, kupiga kopi, kuuza nk.? Hii maana yake yeye si mmiliki wa kitabu hicho. Lakini pia hata kama amegaiwa bure tayari ameshamiliki, kwani hata mtu akipewa kitu bure huwa amemilikishwa. Hivyo, lazima awe na umiliki kamili wa kitu hicho.

**Inaendelea Uk. 6**

lakini kwa mujibu wa fikra ya hatimiliki hana haki ya kukichapisha nakala zaidi, kupiga kopi, kuuza nk.? Hii maana yake yeye si mmiliki wa kitabu hicho. Lakini pia hata kama amegaiwa bure tayari ameshamiliki, kwani hata mtu akipewa kitu bure huwa amemilikishwa. Hivyo, lazima awe na umiliki kamili wa kitu hicho.

Jambo hili lazima liwe bayana kwamba ikiwa mtu ana mawazo, maarifa au uvumbuzi akauza au kuutoa kwa mwengine kazi yake hiyo ya kifikra, iwe kwa sura ya maandishi kama kitabu, makala au kwa namna nyengine kama sauti kama kutoa muhadhara nk. Basi mzaa mawazo au ubunifu huo hana umiliki tena juu ya kitabu alichouza, au muhadhara alioutoa au chochote alichotawanya bure chenye wazo, ubunifu au fikra alizoandika. Na wale walionunua, kupokea, kusikiliza watakuwa na umiliki kamili wa kitabu, makala au fikra zilizomo.

Kwa hivyo, kwa mujibu wa Uislamu walionunua kitabu huwa wamemiliki na wanaruhusiwa kutoa nakala zozote watakazo, au kama ni wazo au ubunifu kutokana na maandishi hayo au sauti wanaweza kuutumia na kuutanua kwa kuuboresha bila ya idhini ya mtoaji wa asili. Kwa kuwa, kitendo cha kununua kitabu, kupewa bure au kuwa katika muhadhara wa wazi maana yake amemiliki.

Uislamu unachokataza unapotawanya kitabu, makala au muhadhara wa mtu fulani lazima umnasibishe mtoaji wa asili. Na inapotokea umeongeza au kupunguza katika kazi hiyo ni haramu kumnasibisha mtoaji wa asili, kwani atakuwa yeye sio tena mwenye kazi hiyo.

Kwa hivyo, yule ambaye anataka wazo, ubunifu, fikra zake zibakie kuwa zake peke yake na sio za mwengine, abakize katika akili yake au katika makabrasha yake kibinafsi anayohifadhi bila ya kutawanywa hadharani kama kitabu au muhadhara. Katika hali kama hiyo endapo mtu atamuibia makabrasha yake aliyohifadhi kibinafsi kama katika laptop yake, mwenye kufanya hivyo atakuwa ametenda haramu. Lakini makabrasha yakiwekwa hadharani kwa muundo wa kitabu, makala au muhadhara maana yake yapo huru kumilikiwa na wengine na kuyatumia au kuyatawanya kwa namna watakavyo.

4. Dhana ya hatimiliki ni sehemu ya kuibana na kuificha elimu isisambae. Na hilo ni haramu katika Uislamu. Mtume SAAW anasema:

من كتم علماً ألجمه الله يوم القيامة بلجام من نار

*'Atakaye ficha elimu Mwenyezimungu atamvisha hatamu za motoni'*

Katika jambo la aibu ni kuona hata vitabu vya dini ya Kiislamu ati navyo vinashikilia dhana hii batil ya kimagharibi ya hatimiliki vikiandikwa

*"Haki miliki imehifadhiwa hairusiwi kufanya chochote ila kwa idihini ya mtunzi"*

*Saratani– kutoka uk.4*

Kwa msingi huo, hatua na mikakati ya kupambana na saratani ambayo wanasiasa hutoa matamko matamu ya kujifakhiri kwamba ipo kwa ajili ya wananchi, lakini ukweli mwisho wake ni miradi ya kimaslahi ya kibiashara.

Katika Uislamu, huduma zote za kijamii kama sekta ya afya, elimu, maji nk. ni milki na haki ya Umma ambapo kazi ya serikali ya Kiislamu ni kuzitoa huduma hizo kwa raia wote bure kwa kutumia mapato ya mali za Umma kama maadini nk. Amma mtu binafsi akitaka kutumia huduma hiyo kwa taasisi binafsi kama shule au hospitali binafsi sio makossa, lakini hilo haliondoshi jukumu la serikali kama msimamizi, mchungaji na mlezi wa raia kubeba jukumu hilo wakati wote. Mtume SAAW anasema:

"Kila mmoja wenu ni mchunga na kila mchunga ataulizwa juu ya uchunga wake."

Dola pekee ambayo ina uwezo na ghera ya kuubeba uchunga huo ni dola ya Khilafah inayopaswa kuanzia katika nchi kubwa za Kiislamu na kuenea ulimwengu mzima.

## Ukoloni wa Sarafu ya Dolari

Dolari ya kimarekani ilianza kuwa sarafu kuu ya kibiashara duniani baada ya Vita vya Pili vya Dunia vilivyoisha mwaka 1945. Hii ilisababishwa na Marekani kuwa muuzaji wa silaha na bidhaa zingine muhimu kwa washirika wake wa Ulaya ambao walimlipa kwa dhahabu, na hivyo kudhoofisha hifadhi zao za dhahabu.

Kwa sababu hii, Marekani ilishawishi na kuua matumizi ya sarafu kwa kiwango cha dhahabu (gold standard) kupitia Makubaliano ya Bretton Wood yaliyofanyika mwaka 1944. Kuanzia hapo sarafu za dunia zikawa hazipimwi tena kwa thamani ya dhahabu, bali sarafu iliyohodhi miamala ya kilimwengu ikawa dolari ya kimarekani.

Huu ndio ukawa mwanzo wa ukoloni wa kiuchumi wa Marekani kupitia sarafu yake ya dolari.

Kupitia sarafu ya dolari, Marekani kama taifa la kibepari, lilichokuwa uongozi wa kimataifa baada ya kudondoka madola ya Ulaya ( Uingereza na Ufaransa) imeweza kupora rasilimali za ulimwengu, kwa kuwa katika nadharia ya msingi ya pesa, pesa ambazo hutolewa kwa nchi fulani kutoka nchi nyingine ni deni. Yaani, ikiwa nchi fulani itachapisha pesa, na kisha nchi zingine kutumia pesa hizo, basi




nchi inayochapisha inakuwa inadai nchi inayoitumia.

Kwa mfano, nchi za Afrika zinapotumia dolari ya Marekani, hulazimika zinunue sarafu hiyo kwa bidhaa na rasilimali. Kwahiyo, Marekani huchapisha pesa, yaani dola ya Marekani kisha nchi za ulimwengu hununua noti za dola za Marekani kwa bidhaa, huduma, na rasilimali nyinginezo.

Kwa mujibu wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) mwaka 2021 pekee, jumla ya mzunguko wa fedha za kigeni duniani zilifikia dolari za Marekani trilioni 11.7 na takriban 60% zilikuwa katika dola za Marekani.

Hii inamaamisha Marekani alitumia rasilimali za ulimwengu zenye thamani ya takribani Dola trilioni 7 bure au kudai madeni yenye thamani hiyo kwa nchi mbalimbali. Madeni ambayo Marekani haijatoa bidhaa yeyote kwa nchi hizo.

Hali ya ulimwengu kuhodhiwa na sarafu ya dolari kumepelekea kulazimisha sarafu za nchi nyingine kushuka thamani. Pesa za nchi zote duniani hushuka thamani kwa sababu zimeambatanishwa na bajeti za serikali. Serikali zote duniani hutengeneza upungufu wa bajeti, yaani matumizi zaidi ya mapato ili "kuhimiza" ukuaji wa uchumi na upungufu huo hufunikwa kwa pesa za uchapishaji ambao hufanya ugavi wa pesa kuongezeka na thamani ya pesa kushuka.

Kwa hivyo, thamani ya pesa inayozunguka katika jamii hushuka kwa sababu serikali inachukua kwa kuchapa pesa mpya. Suala hili hutokea kwa Marekani pia ambayo 50% ya pesa zake hutumiwa ndani na 50% hutumika nje ya mipaka yake. Hii inamaanisha 50% ya mapungufu ya bajeti ya Marekani hulipwa na watumiaji wa pesa ya Marekani ambao si Marekani, yaani nchi nyingine. Hali hiyo hulazumika kuwa na upungufu usiokoma na uchapishaji wa pesa usiokoma ambao hupelekea kushuka kwa thamani za pesa za kusikokoma.

Sarafu katika Uislamu chini ya dola yake ya Khilafah lazima iwe katika dhahabu au fedha au au inasibishwe kwa dhamana ya dhahabu au fedha.

Hali hiyo huondoa mfumuko holela wa bei, huleta uimara (stabilitiy) ya fedha kuepusha kupanda na kushuka kwa thamani ya pesa mara kwa mara. Bali kubwa zaidi italeta uhuru wa kibiashara na hatimaye kukomesha ukoloni wa kiuchumi unaotokana na ukiritimba wa sarafu ya dolari ya Marekani.

Taarifa kwa Vyombo vya Habari

## HIZB UT TAHRIR TANZANIA INATOA MWITO KUACHIWA HURU MAHABUSU WOTE 12 WALIOKAMATWA KWA MARA YA PILI

Hizb ut Tahrir / Tanzania inalaani kwa nguvu zote kitendo cha kukamatwa tena mara ya pili kwa wanaodaiwa kuwa watuhumiwa wa ugaidi ambao waliachiwa huru tarehe 4 Machi 2025 baada ya kushikiliwa kwa miaka kumi.

Watuhumiwa wenyewe ni wafuatao:Ali Mohammed Ulatule (70), Khamisi Mohammed Ulatule (61), Nassoro Suleiman Ulatule, Rajab Ali Mohammed Ulatule, Ramadhani Khamisi Mohammed Ulatule, Saidi Abdallah Chambeta, Fadhili Shaabani Lukwembe, Mnemo Qassim Mwatumb, Abdallah Bushiri Kalukula, Khamisi Ally Masamba, Omari Abdallah Makota na Mohammed Hassan Ungando

Watuhumiwa wote hao waliotajwa waliachiwa huru wiki iliyopita baada ya Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kutangaza kwamba haina dhamira ya kuendelea na shauri lao, lakini kwa ukatili bila ya haya vyombo vya dola vimewatia tena nguvuni na kuwaweka mahabusu katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani.

Ni jambo la kuhuzunisha sana kwamba vyombo vya dola vimewaweka tena watu hao mahabusu kwa mara ya pili bila ya kujali misingi ya utu, kwa kuwa mahabusu hao walikwishawekwa mahabusu kabla kwa muda mrefu



bila ya hatia chini ya kisingizio cha dhulma cha "Uchunguzi Unaendelea", ilhali miongoni mwao wakiwa na umri mkubwa, baadhi kutoka familia moja (Namb 1-5) ambao awali walikuwa watu saba, kwa masikitiko makubwa wawili wamefariki wakiwa ndani ya mahabusu. Zaidi ya yote hayo hakuna malipo yoyote ya fidia watakayopewa.

Hizb ut Tahrir Tanzania imekuwa ikisema mara nyingi kwamba Sheria ya Kupambana na Ugaidi ni sheria ya kigeni ya kikoloni yenye misingi ya dhulma ikigubikwa na mengi ya kutia shaka katika miamala yake kwa kesi zinazoitwa za ugaidi kwa Waislamu wa Tanzania na penginepo. Miongoni mwa ya maswala msingi katika uendeshaji wa kesi hizo kesi ni kwanini ushahidi wa kesi hizo hauwasilishwi mbele ya mahkama? Kwanini watuhumiwa hawapewi haki ipasavyo ya kesi zao kusikilizwa kwa muda muwafaka?

Kwanini watuhumiwa hawapewi dhamana?

Kwa nini wakati mwengine watuhumiwa hukamatwa tena mara ya pili baada ya kuachiwa huru? nk.

Jibu pekee linalodhihirika kwa maswala hayo ni uwepo wa ajenda ya kidhulma kwa kisingizio cha kupambana na ugaidi.

Hizb ut Tahrir Tanzania inatoa mwito kwa Waislamu na wapenda haki wote kupaza sauti zao dhidi ya kitendo hiki cha kunajisi haki, pia tunazitaka taasisi zote za kusimamia haki nchni Tanzania kushikamana na maamuzi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa kuwaachia huru mara moja watuhumiwa wote 12.

Kumb: 1446/08

Jumatano 12 Ramadhani 1446 H

12/03/2025 M

**Masoud Msellem**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari**
**Hizb ut Tahrir Tanzania**

